www.ippmedia.com

# Alasiri Online

Alhamisi Machi 28, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-




# Esha

## MTASUBIRI SANA

## SHISHI NA MAVAZI, MMH!



# ASLAY AJIPANGA KWANZA

**Na Mary Kadoke**

STAA Aslay Isihaka amesema amefikia maamuzi ya kuangalia ramaniyasoko la muziki kabla hajaamua kuachia ngoma juu ya ngoma kama alivyofanya hapo awali.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online amesema kwa jinsi muziki ulivyo sasa hauhitaji presha ya kufanya hivyo. Kwa kufanya hivyo, inafanya mtu aandae kazi nzuri itakayofanya vizuri.

"Muziki unakuwa halafu unabadilika na kuna watu wengi wakongwe na wabichi kwenye game wanafanya vizuri kwenye muziki," amesema.

Akiongeza kuwa, "Hivyo hata kama muda kwa muda nilikuwa natoa ngoma mbili, tatu nne, imefika muda sasa wa kukaa na kutoa kitu cha maana kuendelea kufanya vizuri zaidi."

Miongoni mwa ngoma alizofululiza kuachia mwaka jana na kufanya vizuri katika mtandao wa YouTube ni Natamba yenye watazamaji Milioni 7, Ananikomoa Milioni 2, Kwatu Milioni 2 na Subalkheri Milioni 7.

# Kayumba: Kiki ya nini



**Na Mary Kadoke**

MUIMBAJI na mshindi wa Bongo Star Search 2015 Kayumba Asosie amejiweka kwenye rekodi ya wasanii wasiohitaji kiki ili kuwika kimziki akiamini kuwa ubora wa kazi zake ni silaha tosha.

Akifafanua juu ya msimamo wake huo amesema ngoma zake kufanya vizuri ni kielelezo tosha cha juhudi anazofanya kuendelea kufanya poa kwenye game.

Aidha ameongeza kuwa suala la baadhi ya wasanii kuegemea kwenye kiki si baya kwani kila mtu ana njia zake anazoona zinamfaa katika kuingiza pesa.


Sijawahi kufikiria kufanya kiki kwenye muziki wangu maana naamini kwenye kazi zangu sana na hata ukiangalia ngoma zangu huwa zinafanya vizuri na hazitegemei kiki, amesema.

Kila mtu ana njia zake katika kufikisha muziki wake, kuna baadhi ya wasanii wamejijengea hivyo kwamba bila kiki hawawezi kutoa ngoma zao, ameongeza.

Kati ya ngoma alizowahi kutoa na zikawika kwa mashabiki na mitandao ya kijamii kama YouTube ni Bonge la Toto yenye watazamaji 153,000, Mazoea 209,000 na Maumivu 224,000.

Baadhi ya wasanii waliowahi kutumia kiki kama njia ya kukuza kazi zao ni Young Dee ambaye awali zilizuka habari za kuvuta jiko na watu kuamini kuwa ni kweli ameoa.

Hata hivyo ilikuja kugundulika kuwa ni ngoma yake mpya iliyokwenda kwa jina la Naoa ambayo kweli ilimpa promo na mpaka sasa ina watazamaji 330,000 katika mtandao wa YouTube.



# Esha: Mtasubiri sana

**Na Mary Kadoke**

NDOA ya muigizaji Esha Buheti na mume wake bado ipo gado, mwenyewe amethibitisha hilo na kushangazwa na wanaoeneza uzushi kuwa wameachana.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online Esha amewashauri wazushi hao kutafuta kibarua kingine kwani kukesha wakisambaza habari za kuvunjika kwa ndoa yake ni kuonesha jinsi gani hawana kazi ya kufanya.

"Hakuna kitu kama hicho, hatujaachana bado tupo pamoja na hatuna dalili yoyote ya kuachana," amesema.

"Hizi habari wanazitoa wapi? Nadhani anayesambaza ana sababu zake na la kumshauri tu aachanane na sisi atafute ya kufanya," ameongeza.

Hivi karibuni kupitia mitandao ya kijamii hasa Instagram kwa watu kama umbea_chatroom na udaku zilizuka habari za muigizaji huyu kuachana na mume wake wa ndoa aliyebahatika kupata naye watoto wawili wa kike.



# Prince apakua kitu kipya

**Na Anaeli Mbise**


**MWANAMUZIKI wa Bongo fleva Yayah Prince ameachia video ya wimbo mpya inayoitwa Vibaya.**

**Akizungumza na Alasiri Online, mwanamuziki huyo amesema ujumbe ambao unapatikana katika ngoma hiyo unazungumzia mwanamke mzuri mwenye tabasamu safi, na maneno ya kutia moyo katika mapenzi, hivyo wakija kuachana atajisikia vibaya.**

**Ni ngoma mpya namzungumzia mrembo ambaye niko naye katika mahusiano akija kuniacha nitakuwa na ukiwa kitu ambacho kitanichanganya, amesema Yayah.**

**Msanii huyo pia amesema kuwa video ya ngoma hiyo imerekodiwa chini ya director Mariot Alvero wa World Music Promoters.**

**Aidha mwanamuziki huyo chipukizi katika game ya Bongo ya fleva amesisitiza kuwa atapambana katika tasnia ili afike katika level za kimataifa.**



# SHISHI
# na mavazi, mmh!

Na Mary Kadoke

MUIMBAJI na mjasiliamali Shilole maarufu kama Shishi amesema si muda wote atalazimika kutinga mavazi ya stejini, kwani kwa sasa tayari ni mke wa mtu.

Amesema hayo baada ya kutupiwa lawama kuwa hajui kuvaa angali msanii.

Akifafanua zaidi kuhusu msimamo wake huo amesema si muda wote atafanya muziki, hivyo analazimika kuwekeza kwenye familia yake na biashara nyingine kikamilifu.

"Mambo ya kuvaa sijui nini, mimi kwanza ni mke wa mtu lazima nijiheshimu na niwe na stara si kila muda nitavaa kama niko stejini," amesema. "Muziki upo tu na kuna stage itafika hautaweza tena, hivyo inabidi ujiwekeze," ameongeza. Shishi na mume wake Uchebe walifunga ndoa Disemba mwaka jana

Moja ya mahojiano aliyowahi kufanya msanii Lucky Bebe alisema Shishi ni miongoni mwa wasanii wasiojua kujiweka kisanii hususani upande wa mavazi.

Tofauti na muziki kumtambulisha zaidi Shishi, anafanya pia biashara ya kuuza chakula cha asili kupitia mgahawa wake wa 'Shishi Food' jijini Dar es Salaam.

# Mahaba hayana umri- Kinyaiya




Na Mary Kadoke

MUIMBAJI Ben Kinyaiya amezidi kutema cheche kwa wanaoshangaa maamuzi yake ya kuoa mwanamke anayedhaniwa kuwa mkubwa kiumri kwake.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online amesema kama ni suala la umri, haoni haja ya kuwa na mwanamke mdogo asiyejua thamani ya mume.

Hivyo kwa upande wake aliona ipo haja ya kuwa na mwanamke huyo ambaye kwake anatimiza kikamilifu majukumu yake kama mke.

"Utakapoona kuna sehemu moyo wako umeshiba hutajali wengine wanasema nini," amesema.

"Kuna haja gani ya kuwa na mwanamke mdogo ambaye hakujali wala hakuthamini, mimi la kuwaambia tu kwamba hayawahusu," amesema.

Hivi karibuni Kinyaiya alivuma baada ya picha za ndoa na mwanamke anayedhaniwa kuwa mkubwa kwake kuzagaa mitandaoni.

Hata hivyo pamoja na Kinyaiya, kuhojiwa na vyombo mbalimbali vya habari kuhusu habari za mwanamke huyo yaani uraia, kazi yake, hakutaka kuweka wazi kwani ni mtu asiyefahamika sana.

"Mmm mwanamke mbona mkubwa huyu," aliandika baby_ake kupitia ukurasa wake wa Instagram.

"Ben kafuata pesa tu hapo hamna jipya," aliandika mbeawainsta.

# Wakazi roho kwatu



Na Anaeli Mbise

RAPA Wakazi amefunguka kufurahishwa kwa kuchaguliwa na bodi ya Pan Africanism katika utunzi wa album ya Pan Africa.

Akizungumza na Alasiri Online, Wakazi amesema kuwa lengo la album hiyo ni kwa ajili ya kusherehekea siku ya Afrika Mei 25, 2019 ambayo itafanyika nchini Afrika Kusini.

"Nashukuru bodi wameona kipaji changu na kunichagua katika kuandaa album hiyo na tayari sasa ni ngoma moja nimerodi inayoitwa My Heritage," amesema Wakazi.

Mwanamuziki huyo amesema kuwa kwa kushiriki katika utunzi wa album hiyo itasaidia jina kukua zaidi katika anga za kimataifa na hata kufanya kolabo na wasanii wa nje.

Album ya Pan Africa imeshirikisha wasanii mbali mbali kutoka bara la Afrika kama vile Self Keita wa Mali, kundi la Mafikizolo la Afrika Kusini pamoja na Sauti Sol kutoka Kenya.